**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA**


**MKOA WA RUVUMA**
Anwani ya Simu: "**NYASA COUNCIL**"
Simu Na: 025 -2952003
Fax Na: 025 -2952005
Email: ***ps.ded@nyasadc.go.tz***

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S. L. P. 90,
MBAMBA-BAY,
RUVUMA.


**04 – 01 – 2019**

# T A N G A Z O

1. Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa imepokea Fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya itakayo jengwa katika Kijiji cha Nangombo.

2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa anakaribisha maombi ya mafundi kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya wenye uzoefu katika ujenzi kutoka sehemu mbalimbali (kipaumbele kitatolewa kwa mafundi kutoka Halmshauri ya Wilaya ya Nyasa wenye Sifa).

3. Majengo yatakayojengwa ni kama ifuatavyo:-
   i) Jengo la Utawala
   ii) Jengo la Wagonjwa wa nje (OPD)
   iii) Jengo la Stoo ya dawa
   iv) Jengo la Maabara
   v) Jengo la vipimo vya mionzi (X-ray)
   vi) Jengo la kufulia nguo (Laundry)
   vii) Jengo la wazazi

4. Waombaji wa kazi ya Ujenzi wa majengo tajwa hapo juu wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo;
   **(a) Aweze kufanya kazi bila malipo ya awali (advance payment)**
   **(b) Awe na uelewa wa kusoma ramani (kutafsiri mchoro).**
   **(c) Awe na akaunti ya Benki.**
   **(d) Awe na vitendea kazi vya ujenzi kama vile pima maji, Kamba, n.k**
   **(e) Awasilishe kazi za aina hizo alizowahi kufanya na kusimamia majengo ya serikali.**
   **(f) Uzoefu wa kazi usiopungua miaka 3**
   **(g) Aandae mpango kazi.**
   **(h) Mwombaji mwenye cheti cha ufundi (masonry) Grade Test au awe amepitia mafunzo ya VETA na vyuo vingine vinavyotambulika na serikali atapewa kipaumbele.**

5. Waombaji wenye nia ya kufanya kazi hii ya ujenzi, wanaweza kupata maelekezo zaidi katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya katika Idara ya Ujenzi na Kitengo cha manunuzi.

6. Taratibu za upatikanaji wa Mafundi zitafanyika kwa njia ya ushindani kwa kuzingatia sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2016.

7. Nyaraka za maombi zinapatika kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa katika Kitengo cha Manunuzi. Fomu zinatolewa kuanzia saa 1:30 Asubuhi mpaka saa 9:30 Alasiri siku za kazi kuanzia tarehe ya tangazo hili.

8. Kotesheni zote katika uhalisia wake (Original) pamoja na nakala moja zinazofanana na zilizojazwa kwa usahihi, kusainiwa kwa mkono na kuwekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi na kuandikwa **LGA/145/018/019/W/22/LOT 1** na jina la jengo husika juu ya bahasha pamoja na anwani MKURUGENZI MTENDAJI(W) , S.L.P 90, MBAMBA BAY.

9. Mwombaji anaruhusiwa kuomba kazi zote saba lakini baada ya tathmini akikidhi vigezo atapewa kazi moja tu.

10. Siku ya mwisho ya kuwasilisha kotesheni ni tarehe **11/01/2019** siku ya Ijumaa kabla ya saa 08:30 mchana. Kotesheni zote zitarejeshwa katika Kitengo cha Manunuzi kabla ya muda wa mwisho ulioainishwa.

11. Ufunguzi utafanyika maramoja baada ya muda wa mwisho ulioainishwa hapo juu, mbele ya Mafundi au wawakilishi wao walioamua kuhudhuria katika ufunguzi wa kotesheni za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya.

12. Maombi yatakayochelewa, Maombi yasiyo kamilika, Maombi ambayo hayatakuwepo siku ya ufunguzi, hayatapokelewa na kuhusishwa katika zoezi la uchambuzi wa kumpata fundi atakae fanya kazi ya Ujenzi.

N.B: Waombaji ni mafundi wa kawaida (Local Fundi) na siyo kampuni za kikandarasi

Dkt. Oscar A. Mbyuzi
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NYASA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P 90, MBAMBA BAY
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA